DEPARTMENT OF HEALTH

# Chanjo ya Johnson & Johnson ya COVID-19: Unachohitaji Kufahamu

## Nakala

[muziki wa kusisimua]

[Masimulizi]

**Chanjo ya Johnson & Johnson ya COVID-19: Unachohitaji Kufahamu**

Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) sasa kinapendekeza chanjo za COVID-19 (Pfizer na Moderna) badala ya chanjo ya Johnson & Johnson ya COVID-19.

**Kwa nini mapendekezo yamebadilishwa?**

Wataalam waligundua kuwa tatizo la nadra la kuganda kwa damu lililotokea baada ya chanjo ya Johnson & Johnson ya COVID-19 lilisababisha vifo vya watu wachache. Ingawa tukio hili ni la nadra, ni hatari sana, na kuna chanjo zingine zinazopatikana ambazo hazina hatari hii. Wataalam wamebadilisha mapendekezo baada ya kukagua utafiti wa sasa kuhusu jinsi Johnson & Johnson hufanya kazi, na usalama wake. Wanaendelea kukagua chanjo zote kubaini usalama wake, na ikihitajika, kubadilisha mapendekezo yao kulingana na utafiti huo. Matokeo yoyote yasiyo ya kawaida au yasiyotarajiwa yenye athari mbaya nadra yatakaguliwa na kushughulikiwa, na watu hufahamishwa.

**Je, itakuwaje ikiwa tayari nimepata chanjo ya Johnson & Johnson?**

Hakuna uwezekano wa kukabiliwa na hali ya nadra ya kuganda kwa damu kutokana na chanjo ya Johnson & Johnson ikiwa zaidi ya mwezi mmoja umepita tangu uchanjwe. Ikiwa mwezi haujaisha, angalia kama una dalili hizi:

- Kuishiwa na pumzi
- Maumivu ya kifua
- Kuvimba miguu
- Maumivu ya tumbo ambayo hayaishi
- Maumivu makali ya kichwa au maumivu ya kichwa ambayo hayaishi
- Kuona ukungu
- Kuchubuka rahisi kwenye ngozi au madoadoa madogo ya damu chini ya ngozi mbali na sehemu ambapo ulidungwa sindano

Ikiwa una mojawapo ya dalili hizi baada ya kuchanjwa, unashauriwa kutafuta matibabu mara moja. Mwambie mhudumu wa afya kwamba ulipokea chanjo ya Johnson & Johnson hivi majuzi. Chanjo ya Johnson & Johnson ya COVID-19 inawalinda watu dhidi ya ugonjwa hatari wa COVID-19; hata hivyo, watu waliopata chanjo moja ya Johnson & Johnson bado wanahitaji kupata nyongeza miezi miwili baada ya chanjo yao ya kwanza. Pfizer au Moderna inapendekezwa kwa chanjo nyongeza.

**Je, ninahitaji kupata chanjo tofauti?**

Huhitaji kuanza upya kwa kutumia chanjo tofauti ikiwa chanjo yako ya kwanza ilikuwa Johnson & Johnson. Ikiwa tayari umepata chanjo nyongeza ya Johnson & Johnson, huhitaji kuchanjwa tena kwa sasa.

**Je, bado ninaweza kupata chanjo ya Johnson & Johnson nikitaka?**

Bado unaweza kupata chanjo ya Johnson & Johnson ya COVID-19 ikiwa hiyo ndiyo chanjo unayotaka. Fahamu kwamba mtu yeyote anaweza kukabiliwa na hali nadra ya kuganda damu baada ya kupata chanjo hii. Hata hivyo, kuganda

hutokea mara nyingi kwa wanawake wenye umri wa miaka 30 hadi 49. Zungumza na mtoa huduma wako wa chanjo kuhusu chanjo hii na hatari zake zinazoweza kutokea.

Chanjo ndiyo njia bora zaidi ya kujikinga wewe na wengine dhidi ya COVID-19. Usipochanjwa, zungumza na mtoa huduma wako wa afya au kituo kilicho karibu nawe ili uchanjwe.

[muziki wa kusisimua]

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

2/4/22 (Swahili)

*Ili upate maelezo haya kwa muundo tofauti, piga simu: 651-201-4989*